Haliuzwi
NOVEMBA 24, 2025
/islamicftz
Jumada II 3 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 559
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Kongamano La 4 La Afrika Mashariki
Diamond Jubilee
Disemba 27

# The Islamic Foundation yazindua msikiti mkubwa Kigoma



**600** Msikiti huo wa kisasa uliojengwa kwa ubora mkubwa, una uwezo wa kuchukua takribani Waumini 600



## Rais Mwinyi awasisitiza wananchi kuendelea kuiombea nchi amani

- Mwinyi: Utaratibu watendaji wakuu serikalini wa kusubiri faili ofisini umepitwa na wakati

## Serikali: Miradi ya maendeleo itaendelea licha ya wasiwasi wa wafadhili



Rais Samia alisema Tanzania hapo awali ilifurahia uaminifu mkubwa wa wafadhili, hali iliyowezesha upatikanaji wa fedha kwa urahisi. Hata hivyo, alionya kuwa machafuko ya Oktoba 29 yanaweza kudhoofisha uaminifu huo na kupunguza kasi ya miradi inayoendelea na inayopangwa.



## Mufti Kaabi atoa wito kuliombea taifa amani

**500 wahudhuria kongamano kujadili mchango wa dini katika maendeleo**

## Kilichojificha nyuma ya mpango wa amani wa Marekani huko Gaza




**HABARI**

NA MWANDISHI WETU

DAR ES SALAAM

# Serikali: Miradi ya maendeleo itaendelea vyovyote iwavyo

■ **Kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa kuwaapisha mawaziri wapya Dodoma wiki iliyopita, ilikuwa na lengo la kuwahakikishia Watanzania kwamba serikali ina "Mpango B" iwapo baadhi ya washirika wataondoa au kupunguza msaada.**



## Sh56.49Tril

**Bajeti ya Tanzania ya mwaka 2025/26, iliyopitishwa Juni, ni Sh56.49 trilioni. Kati ya hizo, Sh40.47 trilioni zinatarajiwa kutoka kwenye mapato ya ndani, huku ruzuku kutoka nje ikiwa Sh1.07 trilioni, na mikopo ya ndani na nje ikiwa Sh14.95 trilioni.**

Serikali ya Tanzania imewahakikishia wananchi kwamba miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa itaendelea kama ilivyopangwa licha ya wasiwasi ulioibuliwa na baadhi ya washirika wa maendeleo kufuatia machafuko ya uchaguzi wa Oktoba 29.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema nchi inafadhili miradi yake mikubwa kwa kutumia fedha za ndani na itaendelea kufanya hivyo hata kama baadhi ya washirika watazuia kwa muda utoaji wa fedha.

"Tunatumia fedha zetu wenyewe kujenga miradi hii. Tukipata fedha kutoka nje, tunakopa na kulipa baadaye," alisema.

Alisema Serikali inakusudia kuendeleza miradi kwa namna yoyote kwa sababu miradi inayoendelea italeta manufaa makubwa ya kiuchumi. "Tanzania sasa ni miongoni mwa nchi zinazopiga hatua za haraka kiuchumi. Wengi wanashangaa kuona nchi ambayo ilishawahi kuwa na changamoto sasa ikiunganishwa na Dodoma kupitia SGR," alisema.

Alisema ni bahati mbaya kwamba baadhi ya watu hawatofautishi kati ya mkopo na ruzuku. "Tunakopa na tunalipa, ndiyo maana sehemu kubwa ya mapato ya ndani inaelekezwa kulipia deni. Tunafanya hivyo kwa sababu tulikopa kujenga Reli ya Kisasa (SGR), barabara, kupanua upatikanaji wa maji na umeme, pamoja na kuboresha huduma za afya," alisema Msigwa.

Kuhusu kauli za washirika wa maendeleo yaliyoonesha kutofurahia baadhi ya mambo, alisema anaamini mazungumzo yataondoa wasiwasi huo. "Hii si mara ya kwanza washirika wa maendeleo kutoa kauli kama hizi. Lakini tunakaa, tunazungumza, na mambo yanaendelea," alisema.

Msigwa alisema kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa kuwaapisha mawaziri wapya Dodoma wiki iliyopita, ilikuwa na lengo la kuwahakikishia Watanzania kwamba serikali ina "Mpango B" iwapo baadhi ya washirika wataondoa au kupunguza msaada.

Katika hotuba hiyo, Rais Samia alisema Tanzania hapo awali iliaminika kwa wafadhili kwa kiwango kikubwa, hali iliyowezesha upatikanaji wa fedha kwa urahisi lakini sasa imani huenda ikawa imetetereka kidogo kwa sababu ya machafuko ya Oktoba 29 .

"Kilichotokea kimetutia doa, na huenda kikapunguza uwezo wetu wa kupata rasilimali. Hivyo tunapaswa kutumia tulichonacho kuvutia fedha zaidi ili miradi tuliyoiahidi yakamilike kwa haraka," alisema.

Aliwataka mawaziri walioteuliwa kuongeza juhudi katika kutafuta fedha, akisisitiza kwamba hatavumilia utendaji duni. "Waziri yeyote atakayeshindwa kutimiza wajibu wake ataondolewa," alisema.

Bajeti ya Tanzania ya mwaka 2025/26, iliyopitishwa Juni, ni Sh56.49 trilioni. Kati ya hizo, Sh40.47 trilioni zinatarajiwa kutoka kwenye mapato ya ndani, huku ruzuku kutoka nje ikiwa Sh1.07 trilioni, na mikopo ya ndani na nje ikiwa Sh14.95 trilioni.

Miongoni mwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa ni treni za mijini katika njia zilizoinuliwa Dar es Salaam na Dodoma, zikianzia Kawe, Mbezi, Mlimani City na Kariakoo, huku tawi moja likitoka Bibi Titi Road hadi Ali Hassan Mwinyi Road. Dar es Salaam pekee inatarajiwa kuwa na mtandao wa reli ya mijini wenye urefu wa kilomita 160, huku mpango wa vituo vya SGR ukijumuisha kilomita 105 za reli ya mijini.

جمادى ثاني

# HABARI KIGOMA

NA MWANDISHI WETU

Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, **Aref Nahdii,** ameahidi kuipatia Jumuiya ya Kuhuisha Tabia za Kiislamu (JAI) mkoa wa Kigoma gari la kubebea wagonjwa ili kurahisisha shughuli zao.

**Nahdi** alitoa ahadi hiyo alipotembea Hospitali ya Rufaa ya Kigoma hivi karibuni kuangalia shughuli za matibabu zinazoendelea hapo.

Katika ziara hiyo, **Nahdi** alipata fursa ya kukutana na wanaJAI na watumishi mbalimbali wa hospitali hiyo.

Baada ya ziara hiyo, **Nahdi** alihudhuria ufunguzi wa msikiti mkubwa uliojengwa na taasisi yake ya The Islamic Foundation uitwao Masjid Imaan.



HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU



# Mufti Kaabi ataka Waislamu kuliombea taifa

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, amewataka Waislamu kumuomba Mwenyezi Mungu aliepushe taifa na kila aina ya shari na kulijaalia amani ya kudumu.

Katika taarifa yake, Mufti ameikumbusha jamii umuhimu wa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema mbalimbali alizowajalia wananchi, ikiwemo amani na utulivu ambao umeendelea kuitawala Zanzibar.

Akifafanua njia za mahsusi za kumuomba Mwenyezi Mungu, Kaabi alihimiza Waislamu kufunga Sunna za Jumatatu na Alhamisi na kukusudia ibada na dua, akisisitiza kauli ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) isemayo: "Watu wa aina tatu dua zao hazirejeshwi: Mfungaaji mpaka atakapofungua..." kama ilivyonukuliwa na Imamu Tirmidhi.

Katika kuonesha mfano, Mufti alisema dua maalumu ya kuliombea taifa amani na utulivu imepangwa kufanyika siku hiyo ya Jumatatu katika Msikiti wa Mwembe Shauri, mara tu baada ya Swala ya Adhuhuri.

Mbali na wito huo, Mufti Mkuu amewaombea kheri wanafunzi wote wanaofanya Mitihani ya Kidato cha Nne mwaka huu, akiwatakia utulivu wa fikra, wepesi na mafanikio mema katika mitihani yao.

# 500 wahudhuria kongamano kujadili mchango wa dini katika maendeleo

Zaidi ya watu 500 kutoka mataifa mbalimbali ya ndani na nje ya bara la Afrika wamekutana kwa siku mbili jijini Arusha kwenye kongamano la kujadili kuhusu mchango wa dini katika uchumi na maendeleo, wengi wakifurahia amani na utulivu walioushuhudia nchini tangu kuwasili kwao siku chache zilizopita.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya washiriki hao kutoka nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Senegal, wamewataka Watanzania kushikilia kwa nguvu neema ya amani waliyobarikiwa na Mwenyenzi Mungu.

Mmoja wa washiriki hao, Ogi Kabongo ambaye ni mkazi wa Kinshasa nchini DRC, ameeleza athari za ukosefu wa amani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, akiwataka Watanzania kudumisha amani ya Tanzania kwa gharama yoyote ile kwani ukosefu wa amani unazorotesha na kuua kabisa ustawi na maendeleo ya wananchi. Nae Fransis Owusu kutoka nchini Senegal ameitaka jamii kuendelea kuiombea amani Tanzania, akisema amani hiyo mara zote imekuwa msingi muhimu wa maendeleo na kiwezeshi kikubwa cha mafanikio katika shughuli za kiuchumi.

جُمادى ثاني

HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

# Rais Mwinyi awasisitiza wananchi kuendelea kuiombea nchi amani



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na Wananchi kwa ujumla kuendelea kuiombea Nchi amani na kudumisha mshikamano.

Akizungumza leo tarehe 21 Novemba 2025, mara baada ya kujumuika na Waumini katika Sala ya Ijumaa iliyosaliwa Masjid Rashidin, Dole Sokoni, Mkoa wa Mjini Magharibi, Alhaj Dkt. Mwinyi amesema kila mwananchi ana wajibu wa kutumia nafasi yake kuhimiza na kukumbusha umuhimu wa Amani nchini.

Ameeleza kuwa ni neema kubwa kuona Amani imedumu kabla, wakati na baada ya Uchaguzi, jambo linalopaswa kuendelezwa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuendeleza dua na ibada.

Aidha , Rais Dkt.Mwinyi amesema kuwepo kwa Amani kunaiwezesha Nchi kutekeleza kikamilifu mipango ya Maendeleo katika nyanja mbalimbali, na ameunga mkono tangazo la siku ya Jumatatu tarehe , 24 Novemba 2025 kuwa siku maalum ya Waumini kufunga na kuiombea Nchi Amani.

Halikadhalika, Rais Dkt.Mwinyi ameeleza kwamba madhara ya kukosekana kwa Amani ni makubwa, ikiwemo kupungua kwa upatikanaji wa chakula, kupanda kwa bei za bidhaa, na kuongezeka kwa misukosuko ya kijamii, hivyo umuhimu wa kuiombea Nchi Amani haupaswi kubezwa.

Katika hatua nyingine, Alhaj Dkt. Mwinyi amewaomba Waumini wa Dini ya Kiislamu kuwaombea dua Viongozi Wakuu wa Serikali, ili waweze kutekeleza majukumu na ahadi zao kwa uadilifu na mafanikio, akibainisha kuwa dhamana waliyopewa ni kubwa na ina hitaji msaada wa Mwenyezi Mungu.





NA MWANDISHI WETU

# Dk Mwinyi: Utaratibu wa kusubiri faili ofisini umepitwa na wakati

**“Utaratibu wa kusubiri mafaili ofisini umepitwa na wakati na uongozi wa sasa unahitaji watumishi wenye kasi, ubunifu na utayari wa kuwasikiliza wananchi moja kwa moja.**

Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema sasa si muda wa watendaji wakuu wa Serikali kukaa ofisini kusubiri kuletewa mafaili, badala yake wawafuate wananchi kutatua changamoto zao huko walipo.

Alisema hayo jana, baada ya kuwaapisha makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu aliowateua juzi, kwenye hafla iliyofanyika viwanja vya Ikulu, Zanzibar.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano Ikulu, imemnukuu Dk Mwinyi akisema Serikali haitavumilia mtendaji anayeshindwa kwenda maeneo yenye matatizo, kwani imezoeleka mara nyingi watu hukaa ofisini kusubiri mafaili bila ya kutoka nje.

Alisema utaratibu wa kusubiri mafaili ofisini umepitwa na wakati na uongozi wa sasa unahitaji watumishi wenye kasi, ubunifu na utayari wa kuwasikiliza wananchi moja kwa moja.

“Kuna tabia ya watu kukaa ofisini wakisubiri mafaili waletewe, huo si utendaji tunaoutaka katika awamu hii, tunahitaji viongozi wanaotembea, wanaofuatilia na wanaotatua changamoto kwenye maeneo husika,” alisema.

Dk Mwinyi alisema ipo mifano ya matatizo madogo lakini yanakaa muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi kutokana na watendaji kukaa ofisini.

“Nadhani itoshe sasa, kwani wananchi wa nchi hii wana matarajio makubwa na sisi. Mimi nitakuwa mmoja katika kuhakikisha yeyote yule ambaye hatekelezi majukumu yake, basi anatupisha kwani lengo letu ni kuona yale tuliyoahidi yanatimia,” alisema.

Aliwasisitiza watendaji kutumia nafasi walizopewa kuboresha utoaji huduma kwa umma, sambamba na kuongeza uwajibikaji katika taasisi zao. Aliahidi kufanya kikao kazi na watendaji wote aliowateua na wale wa zamani, wakiwamo mawaziri kuzungumzia matarajio yake katika utekelezaji wa shughuli za Serikali wanapoanza awamu ya pili ya utendaji wake.

## Nyenzo tano za kazi

Dk Mwinyi alisema vitendea kazi vikuu kwa awamu ya pili ya Serikali ya awamu ya nane ni vitano, ikiwamo ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2025/2030.


Alisema ni lazima kila mtu aangalie sekta yake inasemaje katika ilani na kupanga mpango kazi wa kuhakikisha inatekelezwa kwa asilimia 100.

Nyenzo ya pili, alisema ni kuisoma hotuba aliyoitoa akizindua Baraza la 11 la Wawakilishi, kwa kuwa kuna maeneo mengi ambayo amezungumza na yote yanataka utekelezaji, zikiwa ni ahadi alizotoa.

Dk Mwinyi alisema ahadi alizotoa kipindi cha kampeni kwa wananchi ni nyenzo ya tatu, akieleza ofisi yake itatoa orodha ya ahadi hizo na kila taasisi na wizara inapaswa kuangalia maono yake kwa madhumuni ya kujipanga na kutekeleza kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Nyenzo ya nne ni Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar na ya tano ni Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, hivyo wakijipanga vizuri katika utekelezaji wa maeneo hayo, hana shaka kwamba watakidhi matakwa ya wananchi ambayo waliyasema sana kipindi cha kampeni.

“Kwangu mimi zile ni ahadi na muungwana akiahidi anatekeleza, hivyo ninyi ndio watendaji na mnatambua majukumu yenu katika wizara na maofisa masuuli katika wizara zenu,” alisema.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Balozi Dk Emmanuel Nchimbi akifanya mazungumzo na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi Ikulu, Zanzibar jana.Picha na Ikulu

HABARI KIGOMA

NA MWANDISHI WETU




**600**

**Msikiti huo wa kisasa uliojengwa kwa ubora mkubwa, una uwezo wa kuchukua takribani Waumini 600**

# The Islamic Foundation yazindua msikiti mkubwa mkoani Kigoma

**■ Katika uzinduzi huo uliofanyika siku ya Ijumaa, Khatib, alikuwa Amir wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zubeir, aliyepanda jukwaani na kutoa hotuba yenye mafunzo na mwanga wa kiimani.**

Taasisi ya The Islamic Foundation imezindua msikiti mpya uliopo Kigoma Mjini, eneo la Mwasenga, unaojulikana kama Masjid Imaan.

Msikiti huo wa kisasa uliojengwa kwa ubora mkubwa, una uwezo wa kuchukua takribani Waumini 600, hatua inayotarajiwa kuboresha mazingira ya ibada na kukuza ustawi wa kiroho katika jamii ya Kigoma.

Katika uzinduzi huo uliofanyika siku ya Ijumaa, Khatib, alikuwa Amir wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zubeir, aliyepanda jukwaani na kutoa hotuba yenye mafunzo na mwanga wa kiimani.

Alisisitiza umuhimu wa kuitunza nyumba ya ibada, akiwataka Waumini na wakazi wa Kigoma kuhakikisha msikiti huo unahifadhiwa, unasafiwa na unatunzwa kwa manufaa ya sasa na ya vizazi vijavyo. Aidha, alikumbusha juu ya wajibu wa kila raia katika kulinda amani ya nchi, akisema kuwa amani ni nguzo kuu ya maendeleo na ustawi wa jamii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, alieleza kuwa ujenzi wa Masjid Imaan ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ambazo TIF ilitoa kwa wakazi wa Kigoma. Alisema kuwa msikiti huo mkubwa ni mwanzo tu wa miradi mingi mikubwa inayotarajiwa kufanywa na taasisi hiyo katika mkoa huo.

Nahdi pia alibainisha kuwa hatua zinazofuata ni pamoja na ujenzi wa chuo cha dini, shule za msingi, na miradi mingine muhimu ya kijamii itakayochangia elimu, malezi na maendeleo ya wakazi wa Kigoma. Aliahidi kuwa TIF itaendelea kushirikiana na jamii katika kuimarisha ustawi wa kijamii na kiimani.

Uzinduzi wa Masjid Imaan umepokelewa kwa shangwe na matumaini makubwa na wakazi wa Mwasenga, ambao wamesema kuwa mradi huo umefungua ukurasa mpya wa maendeleo ya kiroho na kijamii katika eneo lao.




# MATUKIO KATIKA PICHA

NA ABDULRAHMAN OMAR

## The Islamic Foundation yazindua msikiti mkubwa Kigoma













MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Matamko ya viongozi wa dini na siasa yanavyojenga au kubomoa taifa

**Katika historia ya mataifa mengi, sauti za viongozi wa dini na wanasiasa zimekuwa na nguvu kubwa katika kuunda fikra na mwelekeo wa jamii. katika zama hizi ambapo uelewa wa wananchi umekuwa kutokana na urahisi wa usambazaji taarifa kupitia mitandao ya kijamii, maneno ya viongozi hawa yanabeba uzito mkubwa kuliko wakati mwingine wowote ule Ni katika muktadha huo ndio tunakutana na matamko au kauli za viongozi wa dini na siasa pia wamaokemea, kushauri au kuonya Serikali, jambo ambalo aghlabu huibua mitazamo tofauti kuhusu mustakabali wa nchi. Makala hii inajadili athari – hasi na chanya, faida na changamoto zake za matamko hayo.**

## Athari chanya: sauti za kujenga

Miongoni mwa athari chanya ni kuwa matamko hayo yanawaweka viongozi wa dini na siasa mstari wa mbele katika kuikumbusha Serikali itimize na itekeleze wajibu wake kwa hekima na busara. Qur'an inasisitiza wajibu huu: ***"Na liwepo kundi miongoni mwenu linalolingania heri, kuamrisha mema na kukataza maovu..." [Qur'an, 3:104].***

Mwanafalsafa wa dini, Prof. John Mbiti, aliwahi kusema: "Jamii haiwezi kusonga mbele bila sauti zinazoikumbusha wajibu wake kwa binadamu kauli inaonesha kuwa viongozi ni kioo cha maadili na dira ya jamii.

Pili, matamko yenye mafunzo na rejea sahihi huongeza uelewa wa watu kuhusu haki, wajibu na hali halisi ya nchi na viongozi wake. Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) alisema: "Kila mmoja wenu ni mchunga na kila mchunga ataulizwa kuhusu kile alichokichunga." [Bukhari na Muslim].

Hivyo basi, viongozi wanapowafundisha watu mambo kwa hekima na uadilifu, wanatimiza jukumu lao la kijamii.

Faida ya tatu ni kuchochea mageuzi na ujenzi siasa safi. Wakati mwingine, matamko ya viongozi huleta marekebisho muhimu katika sera na uongozi, iwapo tu ukosoaji huo unakuwa ni wa hekima.

Kwa sababu hiyo, Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie), katika hadith iliyosimuliwa na Shuraiyh bin Ubaid aliweka muongozo mahsusi kuhusu namna ya kuwasilisha malalamiko au kutoa nasaha kwa watawala: "...Mwenye kutaka kumshauri mwenye mamlaka juu ya watu, basi asiutoe ushauri wake huo hadharani; bali amshike mkono (mtawala) na amuoneshe faraghani. Akikubali, basi ndivyo; na asipokubali, basi ametimza wajibu wake." [Ahmad].

Hii inaonesha kuwa ukosoaji si mwiko wala si dhambi, lakini una adabu zake, protokali yake, maadili na utaratibu wake katika Uislamu.

## Athari hasi: sauti za kuvuruga

Hata hivyo, matamko na kauli za viongozi wa dini pia zinaweza kuleta migawanyiko ya kijamii na kisiasa. Viongozi wanapotoa matamko yenye uchochezi au upendeleo fulani uliopitiliza, jamii hugawanyika. Qur'an inaonya: ***"Na fitna ni mbaya kuliko kuua." [Qur'an 2:191].*** Lugha ya mfarakano huathiri umoja wa kitaifa na kuharibu misingi ya maelewano.

Kadhalika, matamko na kauli za viongozi yanaweza kuchochea misimamo mikali. Hii hutokea pale viongozi wa dini wanapozungumza kwa jazba, wakichochea hisia kali. Kauli hizo hutengeneza wafuasi wenye msimamo mkali wasiotumia mantiki. Mtume alisema: "Upole hauwi kwenye kitu ila hukipamba..." [Muslim].

Athari nyingine hasi ya kauli za viongozi wa dini ni kutia doa heshima ya taasisi na kuaminika, hasa pale viongozi wanapochanganya maslahi yao binafsi na wajibu wa kitaifa au wa kiroho. Mwanazuoni mashuhuri, Prof. Ali Mazrui, alionya: "Ukichanganya dini na siasa bila busara, unaweza kupoteza heshima ya dini na ukashindwa kupata tija ya siasa."

Pia, matamko ya viongozi yanaweza, yasipotafitiwa vizuri, huweza kueneza taarifa zisizo sahihi. Katika ulimwengu wa leo wa matumizi makubwa ya akili mnemba na kukithiri kwa taarifa feki, tamko la kiongozi lisilo na rejea linaweza kupotosha umma.

Qur'an inasisitiza: ***"Enyi mlioamini, anapokujieni fasiki na habari yoyote ile, basi (kwanza) ichunguzeni..." [Qur'an, 49:6].***

## Namna ya kuzuia athari hasi za matamko

Kuna mambo kadhaa naweza kuendekeza kuzuia athari hasi za matamko ya viongozi wa dini, ikiwemo kujenga majukwaa la majadiliano ya kitaifa. Tunashauri, serikali, viongozi wa dini, siasa, wasomi na wananchi wanapaswa kuwa na utamaduni wa mazungumzo ya mara kwa mara ya kuondoa mifarakano.

Njia nyingine za kudhibiti matamko hasi ni kusimika uongozi wenye busara na maadili. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Kwa anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na aseme yaliyo mema au anyamaze." [Bukhari]. Huu ni msingi wa uongozi wa busara ambao viongozi wa dini wanapaswa kuuzingatia.

Elimu ya elimu nayo ni muhimu sana. Wananchi wanapaswa kufundishwa namna ya kuchambua taarifa, kutofautisha hoja sahihi na hisia, na kutambua propaganda uchwara.

Nihitimishe kwa kusema kuwa maneno ya viongozi wa dini na siasa yanaweza kuwa nguvu ya kujenga au sumu ya kubomoa. Ni lazima yawekwe katika mizani ya uadilifu, maadili na weledi. Mwanaharakati wa fikra za kijamii, Dkt Cornel West, alisema: "Uongozi wa kweli ni kusema ukweli kwa upendo, si kwa jazba."

Viongozi wakitumia sauti zao kwa hekima, taifa litasonga mbele kwa umoja na ustawi. Wakizitumia kwa mihemko na maslahi binafsi, taifa linaweza kupoteza mwelekeo na kuingia katika migogoro isiyo ya lazima.




# Ghana yaeleza mafanikio kuelekea ujenzi wa huduma za fedha bila riba

Ghana imejitokeza kama nchi inayoinukia katika uwanja wa fedha za maadili barani Afrika, hatua iliyodhihirika wazi kupitia ushiriki wake katika Mkutano wa Kimataifa wa Fedha Endelevu (GEFC) 2025 uliofanyika London.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka tovuti ya News Ghana, ujumbe wa nchi hiyo ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Fedha za Kiislamu Ghana (IFRIG), Dkt. Shaibu Ali, uliwasilisha ramani ya njia ya kujenga mfumo kamili wa fedha zisizotoza riba nchini humo.

Katika hotuba yake iliyopongezwa kwa ufasaha na uchambuzi wa kina, Dkt. Ali alieleza kuwa Afrika inaendelea kuwa ukanda muhimu wa ukuaji wa fedha za maadili, huku mahitaji, uungwaji mkono wa serikali na uelewa kuhusu faida za mifumo ya fedha zisizotoza riba vikiongezeka kwa kasi.

Dkt. Ali alisisitiza kuwa japokuwa Ghana ipo hatua za awali, uungwaji mkono kutoka kwa watunga sera unaongezeka. Alisisitiza kuwa fedha zisizotoza riba ni fursa ya kujenga uimara wa uchumi, kuongeza ujumuishaji wa kifedha na kuvutia mitaji mipya. Tafiti za IFRIG zinaonyesha kuwa 98.4% ya wananchi wako tayari kutumia huduma hizi, huku uelewa ukiwa zaidi ya asilimia 71.

Chanzo: News Ghana



## CBE Noor yatajwa bora huduma za Kiislamu rejareja

**Benki ya Kibiashara ya Ethiopia (CBE) imetangaza kuwa kitengo chake cha huduma za benki zisizotoza riba, CBE Noor, kimetawazwa kuwa Huduma Bora ya Benki Isiyotoza Riba katika Ukanda wa Afrika Mashariki katika Tuzo za 11 za Kimataifa za Benki ya Rejareja ya Kiislamu (11th International Islamic Retail Banking Awards).**

**Kwa mujibu wa tovuti ya stockmarket ya nchini humo, tuzo hiyo ilikabidhiwa leo mjini Karachi, ikiwa ni uthibitisho wa mchango mkubwa wa CBE Noor katika kuendeleza huduma za kifedha zisizotoza riba nchini Ethiopia.**

**Kwa mujibu wa majaji wa tuzo hizo, CBE Noor imeonyesha dhamira thabiti ya kupanua upatikanaji wa huduma hizi kwa makundi mbalimbali ya wananchi, hatua ambayo imeongeza ujumuishaji wa kifedha nchini humo.**

**Aidha, kitengo hicho kimeonekana kuwa kinara katika kukuza na kuimarisha sekta ya benki zisizotoza riba kitaifa, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi na kifedha.**

## Uwekezaji Sukuk ya Al Barakah wavuka malengo

**Sukuk ya Al Barakah ya CRDB Bank imevuka malengo katika kuvutia uwekezaji, jambo linaloonesha nguvu ya ukwasi wa ndani na hamu inayoongezeka miongoni mwa wawekezaji kwa bidhaa bunifu zinazofuata misingi ya Sharia.**

**Sukuk hiyo iliyosajiliwa rasmi kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) Novemba 19, 2025, ilikusanya Sh bilioni 125.4, ikiwa ni asilimia 418 ya lengo. Katika uwekezaji wa fedha za kigeni, ililenga kukusanya dola milioni 5 pekee lakini ikavutia dola milioni 32.3, ikizidi kwa asilimia 646.**

**Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Group, Abdulmajid Mussa Nsekela, alisema matokeo hayo yamevuka matarajio yote, akibainisha kuwa Sukuk hiyo ilivutia zaidi ya wawekezaji 1,000—akiwamo watu binafsi, taasisi, makundi ya kidini, na wawekezaji wa kimataifa kutoka zaidi ya nchi saba.**

**"Kile tulichoshuhudia hakijawahi kutokea. Kukusanya Sh bilioni 125.4 na dola milioni 32.3 si mafanikio tu kwa CRDB Bank, bali pia ni ishara ya kuaminiwa kwa Tanzania," alisema Nsekela.**

# جمادى ثاني

# فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

## Swali: Je biashara ya hisa inayofanyika katika soko la hisa (stock market) ni halali na inaruhusiwa katika Uislamu?

**Jibu:** Uislamu haukatazi biashara ya hisa, mradi biashara hiyo inafuata masharti ya Kiislamu. Tunasema hivyo kwa sababu hisa zinawakilisha umiliki wa sehemu ya kampuni, na mtu anayenunua hisa anakuwa mshirika katika faida na hasara kwenye kampuni hiyo.

Masharti ya uhalali wake ni, mosi, kampuni yenyewe iwe halali yaani haifanyi biashara za haramu kama vile pombe, tumbaku, bangi, kamari, ulevi, mikopo ya riba, kasino na kadhalika.

Pili, uendeshaji wa kampuni uwe halali, ikimaanisha, hata kama kampuni ni ya halali (mfano kampuni ya chakula), ikiwa sehemu kubwa ya mapato au madeni yake ni ya riba, inakuwa tatizo. Katika suala hili, taasisi zilizobobea kama AAOIFI, wameweka vigezo maalum ili kufikia viwango vya kukidhi matakwa ya sharia, kwa mujibu wa Uislamu.

Kigezo cha tatu ni miamala ya soko iwe halali, yaani mtu asijihusishe na kamari, au kununua hisa kwa mkopo wa riba.

Kiufupi, kununua na kuuza hisa ni halali ikiwa kampuni ni halali na hakuna riba au mambo mengine yaliyokatazwa. Lakini ni haramu ikiwa kampuni au mfumo wake una mambo ya riba, pombe, kamari na mengineyo yak ama hayo.

## Swali: Je, ninaruhusiwa kununua kitu kwa mkopo na kulipa kidogo kidogo?

**Jibu:** Imeulizwa kama ni halali kununua kitu kwa mkopo na kulipa kidogo kidogo kama vile kununua gari au friji kwa bei ya juu kidogo kuliko ya kulipa papo hapo, lakini unalipa kwa miezi fulani.

Kwa mujibu wa sharia ya Kiislamu, muamala huo ni halali, kwa sharti kuwa bei iwe imekubaliwa wazi mwanzo (haibadiliki baadaye); pili, mkataba ni mmoja tu hakuna kuchanganya "bei ya kulipa taslimu (cash price)" na "bei ya mkopo" (credit price), kusiwepo riba ya kuchelewa malipo na iwe unaweza kulipa kwa miezi au miaka bila tatizo.

Muamala huu unakuwa haramu ikiwa bei haijulikani ni ipi (cash au mkopo), bei inaongezwa kwa sababu tu ya kuchelewa (riba) au ikiwa kuna adhabu ya riba endapo utachelewa.

Dalili ya uhalali ni pale Bi Aisha (Allah amridhie), anapoeleza katika hadith kuwa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alifanya muamala wa mkopo wa chakula kwa muda kutoka kwa Myahudi na akaweka ngao yake ya chuma kama rehani. [Bukhari 2250], Wanazuoni wamechukua hii kama dalili kuwa mkopo bila riba ni halali.

## Swali: Je, inajuzu kwa jamii yetu kwenda kuchukua mkopo benki isiyokuwa ya Kiislamu kwa ajili ya kununua jengo la ibada?

**Jibu:** Kanuni inasema kuchukua mkopo wa riba ni haramu kabisa katika Uislamu.

Qur'an imekemea riba kwa ukali: "Allah amehalalisha biashara na ameharamisha riba." [Qur'an, 2:275]. Na pia: "Na atakayerejea (katika riba) basi hao ni watu wa Motoni, humo watadumu." [Qur'an, 2:275]. Hivyo basi, hata kama lengo ni zuri, kama kujenga msikiti au jengo la jamii, njia yenye riba haileti uhalali.

Uislamu unazingatia siyo tu lengo bali pia njia ya kufikia lengo. Na bahati nzuri ni kuwa kukusanya michango kama waqf, sadaka, au hisa za halali ikiwemo utafuta Benki ya Kiislamu au taasisi ya fedha inayotoa mikopo ya Murabaha, " (leasing) au Musharaka. Njia nyingine ya kupata pesa kihalali ni kujenga kidogo kidogo kwa michango ya wanajamii. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Ikiwa imeshindikana kabisa kupata njia mbadala ya halali, ni bora kukodisha jengo kwa muda lakini kamwe kamwe kamwe msikope kwa riba

## Swali: Je, Uislamu unaizungumziaje haki ya mke kuhusu mali walizosaidiana na mumewe katika kuchuma (wabia)?

**Jibu:** Hili swali ni la kimsingi, na linagusa misingi miwili mikubwa ya fiqhi ya Kiislamu: haki za mali kwa wanandoa walioishi pamoja na kushirikiana katika kuchuma mali, na haki za urithi baada ya kifo cha mume.

Katika hili, kanuni ya msingi inasema: Kila nafsi ina haki katika kile ilichokichuma." [Qur'an, 4:32]:" Uislamu hautazami tu jina la mali, bali ni nani aliyeshiriki katika kuchuma mali hiyo.

Kwa hiyo, kama mke amechangia kwa fedha, muda, au nguvu katika biashara, kilimo, au miradi ya mali pamoja na mume, na iwapo mchango wake unaweza kuthibitishwa (kwa Ushahidi wa mashahidi au makubaliano), basi anakuwa na hisa halali (kama mali ya ubia) katika kile walichochuma pamoja. Hiyo sehemu ni yake kabla hata ya urithi kuzungumziwa.

Mfano, mke na mume walifanya biashara kwa pamoja na mke aliwekeza 40% ya mtaji au alifanya kazi ya usimamizi yenye thamani hiyo, basi mali hiyo inahesabiwa kama ubia ambapo mke anamiliki 40% ya hisa za biashara hiyo. Hiyo ina maana mali ya mume ni 60% iliyobaki na hiyo ndiyo itarithiwa baada ya kifo chake.

Iwapo kama hakuna ushahidi, lakini ni mchango wa wazi na unaojulikana, Kadhi (hakimu anayehukumu kwa mujibu wa sharia ya Kiislamu) anaweza kukadiria thamani ya mchango wake kwa haki.

Baada ya kifo cha mume, urithi wa mke utapatikana baada ya kugawanya mali ya ubia; na sehemu ya mume iliyobaki ndiyo inakuwa mali yake binafsi. Urithi huo wa mali ya mume utafanyika kwa mujibu wa Qur'an. [4:12]: "Na wao (wake) wanapata robo ya mlichokiacha kama hamna mtoto; na kama mnaye mtoto, basi wao wanapata sehemu ya nane ya mlichokiacha..."

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

HABARI KIMATAIFA

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Kilichojificha nyuma ya mpango wa amani wa Marekani huko Gaza



Mgogoro wa Israel na Palestina una mizizi ya kihistoria inayotokana na kuvunjwa kwa ustawi wa kijamii na kiutawala wa Wapalestina tangu miaka ya 1917 wakati wa Balfour Declaration, kufuatiwa na 1948 (Nakba) ambapo mamia ya maelfu ya Wapalestina walisukumwa nje ya ardhi yao.

Msingi huu wa kihistoria unaonesha kuwa mgogoro haukuanza ulianza kutoka kwenye mifumo ya ukoloni, ubaguzi na migawanyo ya ardhi isiyowashirikisha Wapalestina. Katika muktadha huu, Wapalestina (ambao wengi ni Waislamu) wamekuwa wakipigania haki yao ya kujitawala, ardhi yao ya mababu na hadhi yao kama binadamu, misingi ambayo kwa mujibu wa dini ya Kiislamu ni ya msingi kwa utu na uadilifu wa jamii.

Katika miaka ya karibuni, mgogoro uliingia hatua mpya baada ya vita kubwa za 2023–2025 ambapo Gaza imeshuhudia uharibifu mkubwa uliotajwa na Umoja wa Mataifa kuwa wa kiwango cha janga la kibinadamu.

Uharibifu wa zaidi ya 80% ya miundombinu, kuhamishwa kwa watu zaidi ya milioni mbili, na vikwazo vya kibinadamu vinavyowazuia kupata maji, chakula na huduma za afya, kumetengeneza mazingira ambayo watu wa Gaza hawana tu changamoto za usalama, bali changamoto za kuishi, ukiukwaji unaokinzana na misingi ya huruma, uadilifu na utu kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

Hivi karibuni, mpango wa amani ulioandaliwa na Marekani uliitishwa kupitia azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa likiruhusu kuundwa kwa Jeshi la Kimataifa la Kurejesha Utulivu (International Stabilisation Force -ISF) na Bodi ya Amani (board of peace), limeibua matumaini na mashaka kwa wakati mmoja.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Habari la DW, nchi nyingi zimeunga mkono mpango huu kwa hoja kuwa unaweza kuanzisha njia kuelekea taifa la Palestina. Hata hivyo, kutokuwepo kwa ushiriki wa moja kwa moja wa Wapalestina na lugha tata kuhusu mustakabali wa taifa la Palestina kumeleta wasiwasi wa msingi kwa mataifa kama China na Urusi, pamoja na Hamas ambao wamedai kuwa mpango huo ni aina ya "utekaji wa kisiasa."

Gazeti laThe Guardian limefichua kuwa kuna mipango ya kugawa Gaza katika "green zone" na "red zone", ambapo maeneo yanayodhibitiwa na Israel na vikosi vya kimataifa yataanza kujengwa upya, huku maeneo mengine yakibaki katika uharibifu kwa muda mrefu.

Mfano huu unafanana sana na sera za zamani za maeneo ya kijeshi zilizoshuhudiwa Iraq na Afghanistan, ambapo "green zones" ziligeuka kuwa ishara ya ubaguzi, utenganishi na ukosefu wa suluhisho la kudumu. Kwa mtazamo wa Kiislamu, mgawanyo wa ardhi bila ridhaa ya watu wake unakinzana na misingi ya haki (adl) na ulinzi wa ardhi ya walioonewa.

Jambo linalowatia wasiwasi Wapalestina ni kwamba ISF imepewa mamlaka makubwa ya kiusalama kuliko jeshi la polisi la Palestina litakaloundwa upya, ambalo litaanza na askari 200 tu. Mpangilio huu unatafsirika kama kupunguza mamlaka ya Wapalestina juu ya ardhi yao wenyewe—na hivyo kulinda maslahi ya usalama ya Israel kuliko haki za msingi za Wapalestina.

Tena, mamlaka ya ISF kufanya kazi sambamba na wanajeshi wa Israel katika maeneo ya mpaka, kama ilivyonukuliwa na The Guardian, inaibua hofu ya kuwa mpango huu ni mwendelezo wa udhibiti wa kijeshi badala ya uhuru wa kisiasa. Suala hili linapingana na dhana ya kujitawala na heshima ya taifa lenye imani na utamaduni bayana.

Nchi mbalimbali duniani zimepokea mpango huu kwa mitazamo tofauti: Israel inauona kama fursa ya kuimaliza kabisa Hamas kijeshi; Mamlaka ya Palestina wanauona kama njia ya kupatikana kwa misaada na pengine taifa huru; Hamas wanauona kama tishio kwa mapambano ya ukombozi; na mataifa ya Kiislamu kama Indonesia wamehimiza ushiriki wa Wapalestina na msimamo bayana wa suluhisho la mataifa mawili.

Kutofautiana huku kunathibitisha kuwa mpango huu bado haujaweka mizani ya wazi kati ya usalama wa Israel na haki za Wapalestina, mizani ambayo katika Uislamu hutazamwa kupitia kipimo cha uadilifu, sio nguvu.

جمادى الثاني

## HABARI KIMATAIFA

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Ajali yaua mahujaji wa Umrah 45 Madina



Waumrah 45 kutoka Hyderabad, India, ambao walipoteza maisha katika ajali ya basi Saudi Arabia, wamezikwa kwenye makaburi ya Jannat-ul-Baqi (Al-Baqi) mjini Madina. Mazishi hayo yaliambatana na sala za Janaza zilizofanyika katika Msikiti wa Mtume Muhammad (Masjid an-Nabawi), ikiongozwa na viongozi wa kidini na maafisa wa India na Saudi.

Tukio hili la kusikitisha lilitokea asubuhi ya Novemba 17, 2025, pale basi la waumrah likigongana na tanki la dizeli karibu na Mufrihat, karibu na Madina. Ajali hiyo ilisababisha mlipuko wa papo kwa papo, na basi lilichomwa moto, hali iliyowasababisha abiria wengi kupoteza maisha kwa haraka sana.

Kati ya waathirika hao, kulikuwa na watu wa jinsia zote na watoto — ripoti ya The News Minute inaorodhesha kuwa kati ya waliokufa walikuwa wanaume 17, wanawake 18, na watoto 10. Miili ya marehemu iliwasilishwa kutoka kwenye mortuary hadi kwenye Msikiti wa Mtume ambapo sala ya Janaza ilifanywa, kisha ikapelekwa makaburini kwa mazishi ya heshima.

Wakiongozwa na Gavana wa Andhra Pradesh, Justice S. Abdul Nazeer, maafisa wa serikali wa India walihudhuria mazishi hayo. Balozi wa India Saudi Arabia, Dkt. Suhel Khan, pamoja na Konsuli Mkuu Fahad Suri, walijiunga na familia za marehemu na wapenzi wa waumini katika ibada ya mwisho.

Ripoti zinabaini kuwa 45 waumrah walifariki, huku mmoja akisalimika aliyejulikana kama Mohammed Abdul Shoaib, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Hyderabad. Mohammed alifanikiwa kuvunja dirisha la basi na kuruka nje kabla ya moto kusambaa, na hivi sasa anapatiwa matibabu katika chumba cha wagonjwa mahututi katika hospitali moja huko Saudi Arabia.

Familia za waumrah hao kutoka Hyderabad zimekumbwa na majonzi makali hasa kwa sababu miili mingi iliteketea vibaya, hadi kulazimika kutambuliwa kwa msaada wa teknolojia ya utambuzi wa DNA.

Waathiri wengi walikuwa ni kutoka familia moja kubwa, na majeruhi walisema kuwa watu wengi walikuwa wamelala wakati wa ajali hii, na hivyo hawakuona wakati moto ukianza. Tukio hili ni maafa makubwa kwa waumrah wa India, na limezua maswali juu ya usalama wa usafiri wa waumrah.

---

# Waislamu Ethiopia wapinga ubaguzi kwa watoto wa kike katika elimu

**Baraza Kuu la Masuala ya Kiislamu Ethiopia (SIACE) limeitaka Wizara ya Elimu ya nchi hiyo kuondoa mara moja maagizo mapya yanayoleta ubaguzi dhidi ya wanafunzi Waislamu, hasa wasichana, kutokana na mavazi yao ya kidini.**

**Baraza hilo limesema hatua hizo ni "uvunjifu wa haki za kikatiba" na zinachochea kuingiliwa kwa masuala ya imani ndani ya taasisi za umma.**

**Sheikh Haji Ibrahim Tufa, Rais wa Baraza hilo, ameeleza kuwa mashambulizi ya sera dhidi ya wasichana Waislamu yameongezeka katika miezi ya karibuni, ambapo baadhi ya shule zimepiga marufuku niqabu huku zikiruhusu hijabu, hatua aliyoitaja kuwa "kampeni mahsusi ya kuwatenga Waislamu katika elimu."**

**Taarifa ya Baraza hilo inaonyesha uwepo wa zaidi ya malalamiko 420 yaliyowasilishwa kwao tangu Januari 2024 yakihusiana na vizuizi vya mavazi shuleni. Akifafanua zaidi, Sheikh Ibrahim amesema marufuku hiyo "inalazimisha namna ya kuabudu," jambo ambalo linakiuka Katiba ya Ethiopia, ibara ya 27, inayotambua uhuru wa mtu kutekeleza matendo ya dini bila kubughudhiwa. Takwimu za Human Rights Watch za mwaka 2023 zinaonyesha kuwa zaidi ya 34% ya wanafunzi Waislamu nchini humo wamewahi kukutana na vizuizi vya kiimani katika mazingira ya shule.**

**Ili kukabili kile kinachoitwa "uvunjaji wa mara kwa mara," Baraza limetangaza kuunda kamati ya watu 17 yenye jukumu la kuchunguza matukio hayo kwa kina, kukusanya ushahidi na kuwasilisha mapendekezo ya suluhu endelevu kabla ya mwisho wa mwezi Januari 2026.**

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# Wanafunzi wa Kiislamu tekelezeni wajibu wenu kwa vitendo

Mapema wiki iliyopita, wanafunzi wenye sifa ya kujiunga na vyuo vikuu na vyuo vya kati hapa nchini walianza mchakato wa udahili kwa mwaka wa masomo 2025/2026. Sisi gazeti la Imaan tunawapa kongole wanafunzi wote mliopata nafasi hiyo muhimu, na ambayo tunaamini itarahisisha safari yenu ya kutafuta elimu.

Tunapongeza kuchaguliwa kwenu tukitambua kuwa, elimu si mateso, bali ni sehemu ya mchakato wa kujenga hatma njema ya maisha yenu. Pia, tunawapongeza wazazi na walezi ambao kwa namna moja ama nyingine walikuwa pamoja nanyi katika kuhakikisha mnapata mahitaji muhimu ili muweze kusoma kwa ukamilifu.

Hata hivyo, yafaa mtambue wajibu wenu kama Waislamu juu ya kujiepusha na mambo yote ya haramu na yasiyompendeza Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema: "Mwenye kutenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake, na mwenye kutenda uovu basi ni juu ya nafsi yake vilevile; wala Mola wako Mlezi si mwenye kuwadhulumu waja." [Qur' an, 41:46].

Tunafahamu kwamba hivi sasa kuna wimbi kubwa la mmomonyoko wa maadili kwa watoto na vijana, ambapo tafiti zinaonesha kuwa msingi na tamaduni za malezi kwa wazazi ndiyo chanzo kikubwa cha mmomonyoko huo.

Lakini, nyinyi kama watu wenye malengo maalum, hamna budi kujipamba na sifa ya maadili, tabia njema na kujenga uhusiano mwema na ndugu zenu Waislamu na wasiokuwa Waislamu wakati wote mtakapokuwa vyuoni. Hii ni pamoja na kuendeleza matukufu yote ya Kiislamu ikiwemo kudumisha sala tano.

Ni ukweli kuwa tabia njema inaweza kumshawishi mtu asilimu na ndiyo maana Mtume wetu (rehema za Allah na amani imshukie) alijipamba na mazungumzo ya bashasha kwa watu wote (Waislamu na wasiokuwa Waislamu). Hivyo ni imani yetu mtakuwa chachu ya mabadiliko ya kitabia kwa wanafunzi wenzenu kwa sababu nyinyi mnamfahamu zaidi Muumba wenu.

Haipaswi hata kidogo kutumia vibaya uhuru wa maisha ya chuo kwa kujihusisha na vitendo viovu vitakavyoua ndoto zenu. Kaeni mbali na mijumuiko ya kijamii ambayo inapoteza muda wenu, na epukeni kwenda katika matukio yaliyo kinyume na maadili. Kamwe msijihisi wanyonge na wala msione aibu kudhihirisha Uislamu wenu.

Msilegeze misimamo yenu ya kimaadili ili mlingane na wanafunzi wengine, hata kama ni kwa muda mfupi. Msiwe katika wale wanaotafuta visingizio vya kutupilia mbali misingi ya dini. Mwenyezi Mungu anasema: "Nyinyi mmekuwa umma bora walioletewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu." [Qur'an, 3:110].

Jambo jingine ambalo tunapenda kuwashauri ni kuhusu wazazi. Wapeni faraja wazazi kwa kuwasiliana nao mara kwa mara na muwaheshimu kwa kufanya kile kitakachowaridhisha, na mara kwa mara wakumbusheni wawaombee dua. Msifanye wazazi wenu wajihisi mmewasahau au hamuwahitaji tena.

Maisha yenu binafsi na yale ya kijamii chuoni yanaweza kuathiri masomo yenu, hivyo jikurubisheni zaidi kwa Mwenyezi Mungu ili muweze kumaliza masomo yenu kwa viwango vya juu vya ufaulu.

Kumbukeni chuoni ni mahali pa kupata elimu, ujuzi na maarifa, na si mahali pa anasa, ulevi, uvivu wa masomo, uasherati na matumizi ya dawa za kulevya. Uhuru mlionao haupaswi kutumiwa vibaya, bali uwe fursa ya kujifunza kujisimamia.

MAKALA MAALUM

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Misingi ya kutunza mazingira katika Uislamu

**Uislamu ndiyo dini ya mwanzo kutoa miongozo na sharia za kulinda na kutunza mazingira, ili kuhakikisha usalama, usawa na ustawi wa binadamu, kwa kulinda maji, hewa, ardhi, wanyama, mimea na hata mawe.**
**Allah Mtukufu anasema: "Yeye ndiye aliyekuumbeni kutoka ardhini na akakuamrisheni kuistawisha." [Qur'an, 11:61]. Aidha, Allah amekataza uharibifu wa mazingira kwa kusema "....kuleni na kunyweni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msifanye uharibifu katika ardhi..." [Qur'an, 2:60].**

Katika Uislamu, mazingira yanajumuisha kila kinachomzunguka mwanadamu kutoka katika maumbile ya dunia kama vile maji, hewa, ardhi, wanyama na mimea. Kwa kuzingatia kuwa uharibifu wa mazingira huathiri utekelezaji wa jukumu la utawala (Khilafa) na ustawi wa dunia, Uislamu umelifanya suala la kuhifadhi mazingira kuwa miongoni mwa makusudio makuu ya sharia ya Kiislamu.

Uislamu unahimiza kulinda vyanzo vya mazingira, ambavyo ni maji, chakula, hewa na udongo, na umeyapa umuhimu maji na kuyazingatia kama chanzo cha uhai. Allah Mtukufu anasema: "...na tumejaalia kutokana na maji kila kitu kilicho hai." [Qur'an, 21:30].

Bila maji hakuna maisha kwa binadamu, wanyama, au mimea. Maji yananywesha mimea, wanyama na wanadamu, na Qur'an imeeleza kuwa maji ni neema kutoka mbinguni.

Allah Mtukufu anasema: "Yeye ndiye anayekuteremshieni maji kutoka mbinguni. Katika hayo (maji) nyinyi mnapata ya kunywa, na miti ya kulishia..." [Qur'an, 16:10]. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amekataza kupoteza maji hata wakati wa kuchukua udhu.

Siku moja Mtume (rehema za Allah na amani ziwe juu yake) alimwambia Sa'ad (Allah amridhie) alipokuwa anatumia maji mengi wakati wa kuchukua udhu: "Hii ni israfu ewe Sa'ad." Sa'ad akauliza: "Je, katika kuchukua udhu kuna israfu?" Mtume akamjibu: "Ndiyo, hata ukiwa kando ya mto unaotiririka."

Vilevile, Mtume amekataza kujisaidia haja ndogo kwenye maji yaliyotuama ili kulinda usafi wake na kuzuia magonjwa. Pia ameonya dhidi ya tabia ya kutupa taka, mizoga au uchafu wa viwandani kwenye maji.

Kadhalika, Uislamu unazingatia hewa safi kama sehemu ya maisha, kama yalivyo maji. Na kwa kuwa kila kiumbe hai kinahitaji hewa, Uislamu unahimiza kupanda miti na kuepuka kuikata bila sababu za dharura. Mtume amesema: "Hakuna Muislamu anayepanda mti au kupanda mimea kisha kiumbe chochote – awe ndege, binadamu, au mnyama akala kutoka humo, ila itakuwa ni sadaka kwake."

Pia Mtume amekataza kukata miti kiholela kwa sababu ina faida nyingi, ikiwamo kupendezesha mazingira, kutoa kivuli, kustawisha wanyama, na kusafisha hewa. Amesema: "Msikate miti, kwani ni hifadhi ya wanyama wakati wa ukame."

Aidha, Uislamu unahimiza umuhimu wa kutunza ardhi, kuistawisha, na umekataza kuharibu au kueneza uchafuzi ndani yake. Miongoni mwa njia za kulinda ardhi ni kukataza kujisaidia haja kubwa au ndogo kwenye njia za watu au sehemu wanazopumzika.

Mtume amesema: "Jiepusheni na vitu viwili vinavyosababisha laana." Masahaba wakauliza: "Ni vipi hivyo?" Akasema: "Ni kwa yule anayejisaidia katika njia za watu au kwenye kivuli chao cha kupumzikia."

Kadhalika, miongoni mwa njia za kulinda ardhi na uchafuzi wa mazingira ni kuainisha sehemu maalumu za kujisaidia haja, kama Mtume alivyobainisha: "Mmoja wenu anapotaka kujisaidia haja ndogo, achague (aainishe) sehemu maalum." Vilevile Uislamu umekataza kutupa taka na uchafu kwenye njia au sehemu wanazokaa watu, kwa kuwa kitendo hicho kinawakera wapita njia na kuleta madhara ya kiafya.

Aidha, Uislamu unahimiza kuondoa taka na uchafu barabarani na kwenye nyumba za ibada. Mtume amesema: "Nilioneshwa matendo ya umma wangu, mazuri na mabaya. Miongoni mwa mazuri niliyoyaona ni kuondoa kero njiani, na miongoni mwa mabaya niliyoyaona ni makohozi yaliyomo msikitini..." Pia Mtume amesema: "Kuondoa kero njiani ni sadaka."

Aidha, Uislamu unahimiza kukabiliana na hali ya jangwa kwa kuhuisha na kustawisha ardhi tasa, na kupanda miti. Mtume amesema: "Mwenye kuistawisha ardhi isiyo na mmiliki, yeye ndiye mwenye haki nayo." Kilimo na upandaji ni sehemu muhimu ya kustawisha ardhi na kulinda mazingira.

Mtume amesema: "Kitakaposimama Kiyama na mmoja wenu ana mche wa mtende mkononi mwake, ikiwa ataweza kuupanda (katika siku hiyo), basi na apande." [Ahmad]. Kulinda wanyama ni sehemu muhimu ya mfumo wa maisha duniani, na Allah Mtukufu ameweka manufaa mengi kwa binadamu kutokana na wanyama.

Kadhalika, Uislamu unahimiza kuwafanyia wema wanyama. Mtume amesema: "Hakika Allah amewajibisha kufanya ihsani katika kila jambo; mnapoua (wanyama wanaodhuru) fanyeni kwa wema, na mnapochinja (wanyama wanaoliwa) fanyeni kwa wema; na mmoja wenu ahakikishe kisu chake ni kikali (ili kumuepushia maumivu makali)."

Uislamu umekataza kuwafanyia wanyama ukatili au kuwachezea. Mtume alimlaani mtu aliyemfanya mnyama hai kuwa shabaha ya kujifunza kulenga kwa mishale au silaha nyingine, na kuwatendea ukatili wa aina yoyote Kutokana na mafunzo haya, inadhihirika wazi kuwa kulinda mazingira na rasilimali zake ni jukumu la kisharia katika Uislamu.



# NASAHA ZA WIKI



NA YUSUFU AMINI
0787 503 085

# Hivi kweli hatuzijui faida hizi za sala ya jamaa?

Tunapoangazia falsafa ya ibada katika Uislamu, tunaona sala ndiyo ibada iliyopewa kipaumbele na umuhimu mkubwa ikichukua nafasi ya pili katika mpangilio wa nguzo za Uislamu baada ya tamko la shahada mbili.

Sahaba Abdullah bin Mas'ud (Allah amridhie) amesema: "Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake) alipewa vitu vitatu. Alipewa sala tano, alipewa aya za mwisho wa Suratul Baqarah, na msamaha kwa madhambi ya watu ambao hawamshirikishi Mwenyezi Mungu miongoni mwa umma wake." [Muslim].

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiweka sala katika nafasi ya ibada zinazomuwajibikia Muislamu kila siku ili apate kuwasiliana na Mola wake siku zote, amuabudu yeye peke yake, na asimshirikishe na chochote katika ibada zake.

## Faida za sala ya jamaa

Sala ya jamaa ni faradhi yenye faida nyingi, si tu kwa mtu binafsi bali kwa jamii nzima. Faida ya kwanza wanayoipata wenye kusali jamaa msikitini ni kuzitakasa roho na nafsi zao kutokana na athari mbaya za madhambi. Mwenyezi Mungu anasema: "Hakika ya sala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia mwenye kuisali na mambo machafu na maovu." [Qur'an, 29:45].

Sala ya Jamaa, ambayo huufanya umma ukusanyike pamoja misikitini kila siku mara tano, pamoja na sala ya Ijumaa ambayo huwakutanisha Waislamu kila wiki mara moja, zinatoa taswira nzuri katika jamii, taswira ambayo ni zao la utiifu, nidhamu, upendo, undugu na usawa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Jamii yoyote iliyosimama juu ya sifa hizi inastahiki kuwa juu na hivyo kupigiwa mfano kupitia utekelezaji wa sala, ibada ambayo hutekelezwa katika eneo moja (msikitini).

Kupitia sala ya jamaa tunajifunza nidhamu ya kufuata msimamo wa walio wengi, kwa kile kitendo cha kumfuata Imam katika kila hatua na kisimamo, na pia tunajifunza kupeana nasaha na ushauri pale itakapobainika kuwa mtu ametenda kosa hata kama ana madaraka na cheo kilichotukuka.

Sala ya jamaa inatufundisha nidhamu na kujitolea, kwani inahitaji mtu kufika msikitini kwa wakati ili kuungana na wenzake katika ibada. Kutoka kwa Ibn Umar (Allah amridhie) amehadithia kuwa, Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) amesema: "Swala ya Jamaa inaizidi swala ya mtu peke yake kwa daraja 27." [Bukhari na Muslim]. Katika riwaya nyingine imekuja: "Kuswali kwa Jamaa ni sawa na kuswali swala 25."

Na amesimulia Uthman bin Affan (Allah amridhie) kwamba, Mtume (rehema na amani imshukie) amesema: "Lau watu wangejua yaliyomo ndani ya adhana na safu ya kwanza, kisha wasipate njia ya kulipata hilo ila kwa kura, basi wangepiga kura. Na lau wangejua yaliyomo ndani ya kuwahi mapema, basi wangeshindana. Na lau wangejua yaliyomo ndani ya swala ya Ishaa na Alfajiri, basi wangezien-dea japo kwa kutambaa." [Bukhari na Muslim].

Aidha Mtume amesema: "Mwenye kuswali (sala ya) Ishaa katika Jamaa, basi ni kama aliyesimama nusu ya usiku, na mwenye kuswali Alfajiri katika Jamaa ni kama aliyeswali usiku wote." [Muslim, Abu Daudi na Tirmidhi]. Kwa hiyo, sala ya jamaa haipaswi kupuuzwa asilani, kwani ni fursa ya kipekee ya kupata radhi za Allah.

Inatupasa kujilazimisha kusali kwa jamaa, hasa kwa kuzingatia kuwa sala ndiyo amali ya kwanza ambayo mja atahesabiwa kwayo, na ukamilifu wake ndiyo utakaopelekea kutazamwa kwa amali zilizosalia. Kinyume chake ni kustahiki adhabu ya Jehannam (Allah atuhifadhi).

## Wito wa kusali katika jamaa

Hapana shaka sala ndiyo inayozipa thamani na roho ibada nyingine. Hata hivyo, utafiti unaonesha Waislamu wengi bado wana utamaduni wa kusali siku za Ijumaa na mwezi wa Ramadhan pekee. Kipimo cha kutambua wingi wa Waislamu katika jamii huthibiti katika mahudhurio ya sala ya jamaa misikitini katika nyakati hizo.

Pamoja na ukweli kwamba baba ana wajibu wa kuhakikisha mke na watoto wake wanatekeleza ibada ya sala, inastaajabisha kuona wengi wao wanahudhuria misikitini kwa ajili ya kusali jamaa huku wakiwaacha watoto wao wa kiume nyumbani.

Katika hili, viongozi wa dini, walinganiaji na maimamu wa misikiti wana nafasi muhimu katika kubainisha na kuwafundisha Waislamu umuhimu na faida za sala ya jamaa. Maimamu watumie mbinu sahihi na bora katika kuwabainishia Waumini fadhila na umuhimu wa kuhudhuria misikitini kwa wakati na kushiriki sala za jamaa.

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com







MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

# ZAINAB BINT JAHSH

## Mke wa Mtume

**Wiki iliyopita tulianza kuangalia kisa cha mmoja wa wake wa Mtume, Zainab bint Jahsh (Allah amridhie). Ukiacha nasaba yake, tulianza pia kuangalia kisa chake kilichopelekea hadi kuolewa kwake na Mtume, ikiwa ni amri ya Mwenyezi Mungu ili kuondosha itikadi kwamba, mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa.**

### Qur'an yawajibu wanafiki

Baada ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kumuoa Zainab, wanafiki - kama kawaida yao - walisema sana, "O! Muhamad ameharamisha kuwaoa wake walioachwa na watoto wa kulea, lakini mbona yeye amemuoa mke wa mwanawe Zaidu, inakuwaje?!"

Ndipo Mwenyezi Mungu akawajibu kwa kusema: "Muhammad si baba wa yoyote katika vijana wenu, lakini yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Mitume..." [Qur'an, 33:40].

Katika aya nyingine Qur'an inasema: "...na wala Allah hajajaalia wanenu wa kulea kuwa watoto wenu wa kuzaa. Hayo ni maneno yenu muyanenayo kwa vinywa vyenu (tu), ma Mwenyezi Mungu husema kweli naye huongoza njia ya sawa." [Qur'an, 33: 4].

Aya hizi zinawataka watu kuelewa kwamba, Zaidu si mtoto wa Mtume wa kumzaa kwani wakati huo watoto wa Mtume wanaume walishafariki. Na kwa hali hiyo, hakuna uharamu wowote Mtume kumuoa Zainab, aliyekuwa mke wa Zaidu, mwanawe wa kumlea.

### Utukufu na nafasi yake

Naam, basi Allah akamuozesha Mtume, bi Zainab (Allah amridhie). Alimuoa bila ya walii wala shahidi. Na kwa hilo, akijifakharisha sana mbele ya wake wenziwe, mama wa Waislamu, kama Anas (Allah amridhie) alivyomnukuu akiwaambia: "Nyinyi mumeozeshwa na mawalii wenu, lakini mimi Allah amenioza (kwa tamko lake) kutoka Arshi yake!"

Anasema Aisha (Allah amridhie): "Allah amrehemu Zainab, kwa hakika amepata utukufu mkubwa duniani ambao ni nadra kupatikana. Ameozeshwa na Allah, ambapo Qur'an imetoa tamko rasmi la ndoa yake. Na Mtume ametuambia sisi, 'Itakayekuwa rahisi kukutana nami kwa haraka ni atakayewazidi nyote kwa utoaji sadaka.'"

Kauli hii ya Mtume ilikuwa na ishara kwamba, Zainab ndiye atakayemfuatia Mtume kufa baada yake. Hili lilitimia hili kwani alikufa mwaka wa 20 hijriya kabla ya wakeze wote.

### Zainab mjasiriamali

Zainab (Allah amridhie) alifanya kazi nyingi za mikono zifanywazo na wanawake kama vile kushona, kufuma na kusuka. Pia, alitumia kipato chake kutoa sadaka na kuwasaidia jamaa zake. Vilevile, alijitahidi sana kwa ibada mbalimbali, zikiwemo kuswali, kufunga, dhikr na kusoma Qur'an.

Inasemekana kwamba, Umar alimpelekea Zainab dirhamu elfu 12 kama alivyoidhinisha kwa wake wengine wa Mtume, naye akazichukua na kuzigawa zote kwa wenye shida, mayatima na wajane. Kisha Zainab akamuomba Allah usimfikie tena mgao wa Umar kama huo mara nyingine. [Taz. Rijal wa nisaa hawla rasoul uk 116].

Katika kuelezea utukufu wake aidha, Aisha (Allah amridhie), anasema: "Sikupatapo kumuona mwanamke mwenye dini nzuri, na mchamungu zaidi, na mkweli zaidi, na mshughulikiaji zaidi wa familia yake, na mwenye uaminifu zaidi kuliko Zainab [Rijaal wa nisaa hawla rasoul uk.116].

Kwa upande wa elimu, Zainab hakuwa nyuma. Alipokea hadith nyingi kutoka kwa Mtume, naye akawafundisha wakina Muhamad bin Abdillah bin Jahsh (mtoto wa kaka yake), Ummu Habiba bint Abi Sufiyan (mke mwenziwe), Zainab bint Abii Salama, Kulthoum bint Almustwalaq na wengine wengi.

### Kifo chake

Ilipofika mwaka wa 20 Hijriya katika ukhalifa wa Umar (Allah amridhie), Zainab alifariki dunia huko Madina. Baada ya kuoshwa na kuvikwa sanda, Waislamu –wakiongozwa na Amiril-muominina Umar - walimswalia, na kuzikwa katika viwanja vya Baqii.

Walioingia kaburini kwa ajili ya kumzika walikuwa ni Usama bin Zaid, Muhammad bin Abdullah bin Jahsh na Abdullah bin abi Ahmad bin Jahsh. Allah amridhie Zainab, mama wa Waislamu, na amrehemu, amin.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Kwanini watu hutapika safarini na jinsi ya kuzuia



Kichefuchefu cha safari, ambacho kitaalamu huitwa motion sickness, ni hali inayowapata watu wengi wakiwa kwenye gari, basi, boti, ndege au treni. Mara nyingi huanza kama kizunguzungu, tumbo kugeuka, jasho baridi, na mwisho kutapika. Wengine hupata shida hata kwa safari ya dakika chache. Lakini kwa nini hali hii hutokea, na tunawezaje kujizuia?

Sababu kuu iko kwenye ubongo. Wakati unasafiri, macho yanaweza kuona kana kwamba uko sehemu umetulia. Lakini masikio ya ndani yanahisi mwendo wa chombo unachosafiria. Misuli na viungo navyo vinahisi umekaa tu. Ubongo unapopokea taarifa hizi zinazokinzana, unachanganyikiwa. Hapo ndipo dalili za kichefuchefu zinapoanza.

Watoto wa miaka 2 hadi 12 hupata hali hii zaidi. Wanawake pia huathirika zaidi, pamoja na wajawazito, watu wenye kipandauso, na wale wenye hofu au msongo wa mawazo. Dalili huanza ghafla na zinaweza kuongezeka endapo mwendo unazidi au ukiwa kwenye sehemu yenye hewa nzito.

Habari njema ni kwamba tatizo hili linaweza kuzuiwa kwa mbinu rahisi. Jambo la kwanza ni kuchagua sehemu nzuri ya kukaa. Ukiwa kwenye gari, kukaa mbele hupunguza mtikisiko. Kwenye ndege, sehemu za karibu na mabawa huwa tulivu zaidi. Kwenye boti au meli, katikati ya chombo mara nyingi hakutikisiki sana.

Matumizi ya macho pia yana mchango mkubwa. Kama unasafiri, epuka kusoma vitabu au kutumia simu kwa muda mrefu. Ni bora kutazama mbali, kwenye upeo wa macho. Hii inasaidia ubongo kupata taarifa zinazolingana na mwendo unaoendelea.

Hewa safi ni muhimu. Ukiwa kwenye basi lenye dirisha, kuingiza upepo baridi mara nyingi hupunguza kichefuchefu. Harufu nzito kama mafuta, moshi wa sigara au vyakula vinaweza kuongeza hali hiyo. Ni vizuri kujaribu kukaa mbali na harufu hizo.

Kabla ya safari, kula chakula chepesi na chenye mafuta kidogo. Epuka vyakula vizito, vyenye pilipili au sukari nyingi. Tumbo likijaa sana vinywaji, kama maji mengi, soda au maziwa, huwa rahisi kugeuka na kuongeza kichefuchefu. Kula kidogo lakini mara mbili au tatu kabla ya safari inaweza kusaidia.

Watu wengi hutumia tiba asilia. Tangawizi ni moja ya tiba maarufu zaidi. Inaweza kuliwa kama biskuti, kunywewa kama chai au vidonge. Wengine hutafuna iliki, karafuu au peremende tamu. Jambo hili linafanya mdomo uwe na ladha ambayo inazuia hisia za kutapika.

Ndimu pia hutumiwa na watu wengi. Harufu ya ndimu hupunguza kichefuchefu kwa baadhi ya watu. Mtu anaweza kunusa kipande cha ndimu au kulamba maji ya ndimu kidogo. Si tiba kamili kwa kila mtu, lakini husaidia baadhi ya wasafiri kupata utulivu, hasa kama wanahisi kichefuchefu cha ghafla.

Wapo wanaopata nafuu kwa kunusa mafuta ya mkalatusi au pipi kifua. Harufu hizi huufanya ubongo kujikita kwenye kitu kingine ambacho si mwendo, hivyo kupunguza hisia za kutapika. Hata hivyo, harufu kali sana zinaweza kuongeza kichefuchefu kwa baadhi ya watu, hivyo ni vizuri kujaribu kwa kiasi.

Kuna pia mbinu nyingine ambazo hazina maelezo ya kisayansi lakini watu wengi huzitumia. Baadhi hukaa juu ya kipande cha gazeti au mto laini ili kupunguza mtikisiko. Wengine hutumia barakoa ya macho ili kupunguza msisimko wa kuona. Kutafuna bazoka mara nyingi husaidia kwa sababu inafanya ubongo kuzingatia mwendo wa taya badala ya mwendo wa gari.

Mara nyingine, kubadilisha mawazo husaidia. Kusikiliza qasida tulivu, kuzungumza na mtu, au hata kuimba na watoto kunaweza kupunguza kichefuchefu. Wakati mwingine tatizo hili huongezwa na hofu na fikra nyingi, hivyo kutuliza akili ni muhimu.

Kuna dawa pia zinazosaidia., kama unavyoweza kushauriwa na daktari. Dawa hizi hufanya kazi vizuri zaidi zikimezwa kabla ya safari kuanza. Ni vizuri kushauriana na mfamasia, hasa kama unataka kumpa mtoto.

Ikiwa tayari umeanza kuumwa safarini, pumua taratibu. Fumba macho. Tazama mbali au kaa kimya hadi mwili utulie. Kunywa maji kidogo kidogo. Ukisikia unataka kula kitu, biskuti kavu kama soda crackers zinaweza kusaidia.

Mwisho wa yote, kichefuchefu cha safari ni hali ya kawaida. Hakina maana ya udhaifu. Ni mwitikio wa mwili kwa mwendo. Kwa kutumia mbinu hizi rahisi, safari inaweza kuwa nyepesi, tulivu na hata ya kufurahisha tena.


Sikiliza Radio
Imaan FM
Dar es Salaam 104.5fm
Arusha 90.8fm
Mwanza 106.5fm
Mbeya 90.3fm
Tabora 101.6fm
Ruvuma 94.2fm
Mtwara 90.9fm
Kigoma 92.5fm
/radioimaanfm
MOROGORO
96.3 fm
MSAMVU
twiga
Elimu Bila Mipaka

# MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA



# Viongozi watakapoulizwa walichunga vipi mali za umma

Abu Humayd as–Saidiy (Allah amridhie) amesimulia kuwa, Mtume (rehema na amani zimshukie) alimteua mtu mmoja aitwae Ibn Al–Lutbiyya akusanye zaka kwa watu wa kabila la Bani Sulaym. Al–Lutbiyya aliporejea (baada ya kukusanya zaka), Mtume (rehema na amani zimshukie) alimhoji kuhusiana na mahesabu ya mali aliyokusanya.

Al–Lutbiyya akasema: "Hii ni mali yenu, na hii hapa ni zawadi niliyopewa." Mtume (rehema na amani zimshukie) akamwambia: "Ungekaa nyumbani kwa baba yako na mama yako uone kama ungepewa zawadi hiyo, ikiwa unasema kweli."

Kisha Mtume akatoa khutba, akaanza kwa kumsifu na kumshukuru Allah, kisha akasema: "Ama baada ya haya, mimi nimemtuma mtu miongoni mwenu kufanya kazi katika mambo ambayo Allah amenikabidhi, kisha mtu huyo anarudi na kusema, 'Hii ni mali yenu, na hii ni zawadi niliyopewa.' Kwanini asingekaa nyumbani kwa baba yake na mama yake aone kama angepewa zawadi hiyo?

"Naapa kwa Allah! Hakuna yeyote kati yenu atakayechukua kitu kisichokuwa chake kwa njia isiyo ya halali isipokuwa atakutana na Allah Siku ya Kiyama akiwa amebeba mzigo huo! Kwa hakika nitamjua mmoja wenu Siku ya Kiyama akija mbele ya Allah akiwa amebeba ngamia anayepiga kelele, au ng'ombe anayeunguruma, au kondoo anayelia!'" Kisha Mtume akanyanyua mikono yake hadi makwapa yakaonekana, akasema: "Ewe Allah! Je, nimefikisha (ujumbe)? Ewe Allah! Haya ni macho yangu na masikio yangu yanashuhudia." ***[Bukhari]."***

## Mafundisho ya tukio hili

Sheria ya Kiislamu imeweka mkazo mkubwa juu ya kuwahoji watumishi wa umma, hasa waliopewa madaraka katika yale waliyokabidhiwa kuyasimamia.

Ni wajibu wa kiongozi kuwapa nasaha na maelekezo watumishi wa umma, kuwahoji, pamoja na kuwaonya vikali kuhusu mwisho mbaya wa watawala au viongozi wanaochukua mali au kitu wasichostahiki, ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu, uaminifu na bila dhuluma yoyote.

Kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wa umma kunazuia ufisadi, rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Mtume (rehema na amani zimshukie) alisisitiza uwajibikaji huu kwa sababu kila kiongozi ni mchunga na atahesabiwa juu ya raia wake, kama alivyosema: "Nyote ni wachunga na kila mmoja wenu ataulizwa juu ya wale aliowachunga." [Bukhari na Muslim]. Kiongozi anapowahoji watumishi wake, anakuwa analinda haki za watu, heshima na maadili ya uongozi, na anatafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

## Zawadi yaweza kuwa hongo au rushwa

Uislamu unahamasisha kupendana na kupeana zawadi, kwa kuwa hiyo ni njia bora ya kuunganisha nyoyo na kuimarisha upendo na huruma. Lakini wakati huohuo sheria inamkataza mtumishi wa umma kupokea zawadi inayotokana na nafasi yake kazini.

Sababu ni kwamba, zawadi hiyo inaweza kutumika kama hongo au rushwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili mtoa zawadi anufaike na cheo cha kiongozi huyo kukidhi maslahi yake binafsi. Katika Uislamu, ni haramu kiongozi au mtumishi wa umma kupokea zawadi kwa sababu ya cheo chake, na kufanya hivyo kunachukuliwa kuwa ni kupokea rushwa au kufanya ubadhirifu wa mali ya umma.

Mtume (rehema na amani zimshukie) ametufundisha kuwa, zawadi zinazotolewa kwa sababu ya madaraka ni haramu, na atakayezipokea atakutana na Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama akiwa amebeba mzigo huo. Kupokea zawadi huwafanya viongozi wafuate matakwa ya wale waliowapa zawadi hizo badala ya kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

Zawadi zinapoteza imani ya wananchi kwa viongozi wanaotumia nyadhifa zao kujinufaisha. Vilevile, zawadi husababisha ufisadi na kudhoofisha utawala bora, maendeleo na utoaji haki. Mtume (rehema na amani zimshukie) alionesha uadilifu wa hali ya juu katika uongozi kwa kusimamia haki na uwajibikaji katika utumishi.

Huu ni msingi bora wa uongozi, ambao kila kiongozi anapaswa kuuzingatia, Viongozi wana majukumu mazito ambayo yatauliziwa mbele ya Muumba Siku ya Kiyama. Siku hiyo kila mtu atawajibishwa mbele ya Allah kwa mali yake au madaraka aliyopewa.

Mtume alishughulika na makundi yote katika jamii – masikini, mafukara, yatima, wajane na wengineo wenye uhitaji. Hawa wote walishikwa mkono na kuwezeshwa. Mtume hakuwa kiongozi anayetumia tabaka la wanyonge kujinufausha yeye na familia yake.

## Tabia za viongozi wa sasa

Mazingira ya uongozi kwa sasa yamegubikwa na dhana ya kujinufaisha na kutazama zaidi maslahi binafsi, ambapo kila mtu anayepata fursa anatamani kuitumia kupata uongozi utakaomwezesha kujinufaisha yeye binafsi, iwe kwa kupindi kifupi au kirefu atakachokuwa madarakani.

Dhana hii ndiyo inayopelekea viongozi wengi siku hizi kula rushwa na kupuuza majukumu yao ya kuutumikia umma wanaouongoza. Ni viongozi wachache sana wanaohisi kuwa vyeo walivyonavyo ni dhamana kubwa inayohitaji uadilifu, ni mzigo mkubwa ambao wanapaswa kuubeba kwa uangalifu mpaka watakapoutua.

Viongozi wanapaswa kuwajibika kwa yale waliyoyaahidi kuyasimamia na kuyatekekeza, na hawatakiwi kutumia unyonge wa watu kama nyenzo ya kuwatweza na kusahau ushawishi mkubwa walioutumia katika kupata nafasi walizonazo. Kupitia ahadi mbalimbali wameweza kufika hapo walipo, kwa hiyo wana wajibu wa kusimamia kile walichoamini kuwa wakipewa dhamana ya uongozi watakifanya.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

www.islamicftz.org

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Yajue malezi ya baraza mbili na hatari zake

Wiki mwishoni mwa wiki hii nilikuwa Tanga kwenye shughuli za kifamilia, na nikiwa huko nikatembelea kijiji chetu cha Kivindani kusalimia wazee.
Katika safari yangu, nilibahatika kuhudhuria kikao cha wazee waliokuwa wakipiga soga na mada mezani ilikuwa ni malezi, hususan kiini cha watoto na vijana wa sasa kukosa adabu ukilinganisha na zamani.

Moja ya mapungufu ya kimalezi yaliyoibuliwa ni kile kilichoitwa na wazee ni malezi ya "baraza mbili"; ambapo mzazi au mlezi anasaliti walezi wengine anaosaidiana nao katika kulea kwa kuwa na vikao vya pembeni na mtoto, akimpa faraja baada ya kusemwa katika jumuiya.

Matokeo ya Faraja hiyo ni kuliosha kosa la mtoto na kumfanya ahisi kuwa yeye si mwenye makosa bali mzazi Fulani. Kwa Kiingereza, hali hii huitwa "undermining the other parent" – yaani kumvunjia mzazi mwenza mamlaka na heshima yake ya kimalezi mbele ya mtoto.

Lazima nikiri kuwa yaliyosemwa yana ukweli mwingi sana, na binafsi naweza kukumbuka nyakati kadhaa ambapo nilikaa na mtoto kumpa faraja baada ya kusemwa. Sikuwahi kufikiri kwamba licha ya nia yangu nzuri, yapo madhara yanayoweza kutokea.

Aghlabu, unaweza kumsikia mzazi akisema: "Unamjua baba yako na ukali wake wa kupitiliza. Kila kitu anakibeba kwa uzito mno... Usijisikie vibaya sana, mwache aseme, yataisha."

Au bibi anaweza kusema akimwambia mjukuu wake wa kiume: "We si unajua wanawake tulivyo, usimchukulie sana mamako. Yeye mwenyewe alikuwa hivyo hivyo tu, kivuruge, asikuseme wewe tu."

Kauli hizi zinaonekana kama faraja, lakini ndani yake zinabeba ujumbe mwingine: zinamwambia mtoto kuwa yule aliyemkemea hana hoja, ni mbaya, malezi yake yana upungufu au ni wa ajabu. Hapo ndipo "baraza la pili" linapojengwa. Kwanza kulikuwa na baraza la pamoja la kumkosoa mtoto, kisha linakuja baraza la faragha la kufuta au kupunguza uzito wa kosa.

Wazazi walioachana

Baraza mbili inakuwa na madhara zaidi katika familia za wazazi walioachana. Katika lugha ya malezi ya kisasa, tunazungumza "co-parenting" – yaani wazazi au walezi wanaoshirikiana katika kumlea mtoto, iwe wanaishi pamoja au wametengana.

Msingi wa co-parenting wenye afya ni kutoa ujumbe mmoja thabiti kwa mtoto kuhusu nidhamu, mipaka na wajibu. Ndipo tunapomwambia mtoto, kwa vitendo, kuwa wote tunaangalia maslahi yake, si kushindana kumpendeza.

Tatizo la "baraza mbili" ni kwamba mtoto hapati nafasi ya kujifunza uwajibikaji. Anajifunza ujanja. Anagundua haraka kuwa kuna mzazi "mshirika" na mzazi "adui". Anajua akikemewa na baba, atakimbilia kwa mama apate maneno ya: "Usijali, baba yako ni mkali kupita kiasi." Hapo sheria inageuka kitu cha kujadiliana, si mpaka wa wazi.

Madhara ya baraza mbili

Mtoto anayekulia kwenye mazingira ambapo hana majukumu, hapewi mipaka, na kila kosa linapunguzwa uzito wake, baadaye anaweza kukua bila kuelewa matokeo ya maamuzi mabaya.

Kwanza anaweza kuonekana tu ni "mtoto msumbufu" nyumbani – hataki kazi za nyumbani, hataki kusikiliza, anaona kila anayemkanya ni mbaya. Lakini kadiri anavyokua, hilo linaweza kugeuka kuwa kutokujali maadili kazini, kwenye ndoa, na hata katika mambo makubwa kama ulezi wa watoto wake.

Zaidi ya hapo, "baraza mbili" linaharibu ushirikiano wa walezi. Mlezi mmoja anapojitoa kuwa mkali kidogo kwa ajili ya kumweka mtoto kwenye mstari, halafu mwingine anamuonesha mtoto kuwa ule ukali ni ujinga au ukatili, chuki na kinyongo kati ya wazazi au walezi huanza kujengeka kimyakimya.

Kinachofuata ni kuwa hakuna tena mazungumzo ya kimkakati ya watu wazima kuhusu namna bora ya kunyanyua tabia za mtoto; bali kinachobaki ni mashindano ya "nani anampenda mtoto zaidi".

Suluhisho si kuwa wakali kupitiliza wala kumuumiza mtoto kwa adhabu zisizo na mipaka. La hasha. Suluhisho ni kuheshimiana na kushirikiana kwa kujenga msimamo mmoja thabiti katika malezi.

Malezi ya jamii nzima

Katika muktadha wa Kiafrika malezi si kazi ya baba na mama pekee. Kaka, dada wakubwa, wajomba, mashangazi, bibi, babu na hata majirani – wote ni sehemu ya mnyororo wa walezi.

Zamani ilisemwa "mtoto ni wa jamii". Mtoto akikosea njiani, mjomba au jirani alimkanya na wazazi wakaliunga mkono. "Baraza mbili" linapoingia, tunaanza kumwambia mtoto bibi yenu hawapendi wajukuu zake nyinyi kwa sababu hamjazaliwa na mtoto wake pendwa, bibi yenu ni mchawi na kadhalika. Au yaweza kusemwa: "Mjomba wako anapenda kukusema lakini kawashindwa."

Hapo si tu tunamvunjia heshima walezi wenzetu katika jamii, bali tunabomoa ule ulinzi wa kifamilia na kijamii uliokuwa unamsaidia mtoto kujifunza maadili.

Badala yake, watu wazima – wazazi na ndugu – tunapaswa kujenga "baraza moja". Tukiwa na tofauti kuhusu namna ya kumrekebisha mtoto, tuzungumze faraghani kama watu wazima au tumshirikishe mzee wa familia.

Mbele ya mtoto tuwe na sauti moja: kosa ni kosa, heshima ni heshima. Hapo ndipo methali ya "inahitaji kijiji kizima kumlea mtoto mmoja" inapopata uhalisia, na "baraza mbili" linapoteza kabisa nafasi katika nyumba zetu.



MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Walimu wa madrasa wasomeshwe saikolojia ya elimu

**Kila mmoja wetu anaweza kuwa na mtoto, mpwa, mjukuu au mtoto wa jirani ambaye kila tukimuuliza, "Uko sura gani huko madrasa?" jibu lake halibadiliki mwaka hadi mwaka: "alifu," "alifatahatain," "allaa, balaa, talaa," au waliopiga hatua kidogo husema "alhamdu." Watoto hawa husomea sura zile zile kwa miezi na miaka bila kusonga mbele, wakiishia tu kubadili vitabu vya majuzuu bila maendeleo. Si kwamba watoto hawa hawana uwezo bali lakini ni matokeo ya kurundikwa katika kundi moja, huku mwalimu akitumia mbinu ile ile kwa wote. Mbinu ya ufundishaji inaweza kufaa kwa huyu lakini isifae kwa yule kutokana na tabia zao, na hapa ndio umuhimu wa somo la saikolojia unapokuja.**

**Kuna watoto ni wepesi mno kushika masomo, na akiwa na wasioelewa haraka huchoka na kuanza utundu au kukosa motisha ya kwenda madrasa. Kuna wenye uhitaji maalum ambao mwalimu huhitaji muda wa ziada wa kuwahudumia. Hapo ndipo umuhimu saikolojia ya elimu unaonekana.**

## Maana ya saikolojia ya elimu na faida zake

Saikolojia ya elimu ni tawi la sayansi ya tabia linalochunguza namna watoto wanavyojifunza, sababu za tofauti zao kielimu, jinsi ubongo unavyohifadhi taarifa, vichocheo vya motisha, na mbinu bora za kufundisha kulingana na tabia na uwezo wa mwanafunzi. Kwa kifupi, somo hili linamsaidia mwalimu kumfahamu mtoto, ili aweze kumfundisha kwa ufanisi zaidi.

Katika mazingira ya madrasa, ambako watoto hutoka katika familia, umri, tabia na vipawa tofauti, ujuzi huu ni hazina isiyoweza kupuuzwa. Faida zake ni nyingi ikiwemo kuelewa jinsi watoto wanavyojifunza—kwa kusikia, kuona, kugusa, kurudia, au vitendo na hivyo kuchagua mbinu sahihi za kufundisha.

Mwalimu aliyesomea saikolojia anaweza kugundua uwezo mahsusi wa kila mtoto na changamoto zake na kuandaa mkakati unaomfaa mtoto husika na hata kubadilisha mbinu kulingana na mahitaji ya mtoto, badala ya kutumia njia ile ile kwa kila mtoto.

Pia humsaidia mwalimu kuelewa tofauti baina ya watoto. Hakuna watoto wawili wanaofanana. Wapo wenye uelewa wa haraka, wenye uhitaji wa muda zaidi, wenye changamoto za tabia, na kadhalika.

Saikolojia pia humwezesha mwalimu kuunda mazingira rafiki ya kujifunzia. Watoto hujifunza vizuri wakiwa katika mazingira yenye utulivu, heshima na uwepo wa hisia chanya. Inamfundisha mwalimu namna ya kuunda darasa lenye nidhamu bila ukali, sauti bila vurugu, na umakini bila hofu.

Aidha,saikolojia humsaidia mwalimu kutumia mikakati inayozingatia umri kwani mtoto wa miaka 5 hawezi kujifunza kwa njia sawa na wa miaka 12. Saikolojia inaeleza hatua za ukuaji—kihisia, kijamii na kiakili—na humsaidia mwalimu kupanga masomo kulingana na umri wa mtoto.

Motisha na ushiriki wa wanafunzi ni jambo jingine muhimu. Walimu wengi huzania mtoto asiposoma "hana adabu" au "anaringa." Mwalimu mwenye ujuzi wa saikolojia hutambua visababishi vya ndani: huenda ni hofu, kuchoka, kutengwa, au matatizo ya nyumbani. Anajua namna ya kuamsha hamasa ya ndani ya mtoto badala ya kutumia vitisho.

Saikolojia pia humfunza mwalimu kuepusha kumuumiza mtoto kihisia. Aghlab, kupiga, kubeza au kutukana si mara zote humsaidia mtoto. Inamwongoza kutumia nidhamu jumuishi—kuongea, kuelekeza, kuweka mipaka, kujenga tabia njema na kuwajengea watoto uwajibikaji.

Mwalimu mwenye utaalamu wa saikolojia anaweza pia kushauri wazazi, kwa sababu wakati mwingine tatizo si madrasa tu, bali pia nyumbani. Anaweza kuwapa wazazi mwongozo kuhusu ratiba ya masomo ya mtoto, tabia, au namna ya kumsaidia mtoto aliye na changamoto ya maendeleo. Vilevile, anaweza kutathmini maendeleo ya mwanafunzi. Badala ya kumfundisha mtoto mwaka mzima bila kujua kama ameelewa, hutumia mbinu rahisi za tathmini kama maswali, mazoezi, kusikiliza usomaji, na kufuatilia tabia.

## Nini kifanyike?

Tatizo la msingi ni kwamba walimu wetu wengi wana maarifa makubwa ya dinilakini wanakosa msingi wa falsafa ya elimu, saikolojia ya elimu, mbinu za kufundisha, na mbinu za tathmini. Matokeo yake watoto kusomeshwa kwa mazoea, bila mkakati wa kielimu unaozingatia tofauti za watoto.

Kwa msingi huo, ili kuboresha madarasa zetu, tunahitaji kozi fupi za kuwajengea walimu uwezo kwenye maeneo hayo. Kozi hizi zinaweza kufanyika kwenye misikiti, taasisi za Kiislamu au hata mtandaoni. Mafunzo ya wiki moja tu yanaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Nimalize kwa kusisitiza kuwa hakika, mtoto anapojisikia kueleweka na kufundishwa kwa mbinu inayomfaa, ataipenda Qur'an, ataithamini dini na atasonga mbele kwa kasi anayostahili; na tukiwekeza kwa walimu wetu wa madrasa, tunawekeza katika hatma ya Uislamu wetu.

NA UKHTI FATIMA



# Ushauri wa bure kwa jeshi la wasaka ajira toka vyuo vikuu

Baada ya kuvuka hatua ya mwisho ya masomo ya chuo kikuu, wengi huamini kuwa maisha sasa yatanyooka, kazi itapatikana haraka, na malengo binafsi kufikiwa. Lakini ukweli ni mabadiliko kutoka maisha ya kusoma kwenda maisha ya kazi si rahisi.

Mabadiliko haya yanahitaji maandalizi, uvumilivu, na kuelewa mazingira ya ajira ambayo yanabadilika kila uchao. Hata hivyo, kwa kufuata hatua kadhaa, unaweza kujiweka katika nafasi nzuri ya kufanikiwa kwa haraka.

Hatua ya kwanza muhimu ni kutafakari malengo yako ya kazi. Jiulize unataka kuwa nani katika miaka ijayo. Utaingia kwenye ajira rasmi? Utajijengea biashara yako mwenyewe?

Malengo haya ndiyo dira yako. Yanakuepusha na kuchanganyikiwa na kukusaidia kupima hatua zako kila mwezi au kila mwaka. Hata kama mazingira yatabadilika, kuwa na malengo hukupa msingi wa kufanya maamuzi magumu kwa uthabiti.

Baada ya kujua unachotaka, tafiti wa kina kuhusu soko la ajira. Hili ni jambo ambalo wahitimu wengi hulidharau. Tambua sekta zinazoajiri zaidi, aina za kazi zinazohusiana na taaluma yako, na kampuni zinazofaa uwezo wako.

Vilevile, tumia majukwaa ya ajira mtandaoni, mahafali ya kikazi (career fairs), tovuti za ajira, mitandao ya kijamii ya kitaaluma kama LinkedIn, na kadhalika.

Usiogope kuanza na nafasi za chini ambazo huenda si ndoto yako. Jua kuwa mara nyingi hizi ndizo ngazi za kwanza zinazokujengea ujuzi na mtandao unaohitaji ili kupanda juu baadaye.

Kwa sababu ushindani ni mkubwa, andaa wasifu (CV) ambao unaonyesha utofauti wako. Dunia ya ajira leo inathamini wahitimu wanaoweza kufanya zaidi ya walichosoma darasani. Jumuisha kwenye CV yako mambo kama ujuzi wa ziada, shahada ndogo ndogo za mtandaoni, kazi za kujitolea, miradi binafsi, klabu ulizoshiriki, au hata vipaji maalum. Rekodi hizi huonyesha kuwa wewe ni mtu anayeweza kubadilika, una shauku, na unajituma nje ya mazingira ya darasa.

Kumbuka pia kwamba kupata kazi kunategemea sana namna unavyouza uwezo wako kupitia mahojiano. Hoja nzuri inaweza kupotea kama huwezi kuwasilisha mawazo yako kwa ujasiri. Jifunze maswali ya kawaida katika sekta unayolenga.

Jitayarishe kutoa mifano ya wakati ulitatua tatizo, uliwahi kuongoza kundi, au ulijifunza jambo jipya kupitia changamoto. Mazoezi haya yanaongeza utulivu na kujiamini, mambo ambayo waajiri wengi huyathamini sana.

Lakini ukweli unaobaki ni kwamba si kila aliyehitimu hupata kazi haraka. Wapo wanaokaa bila ajira kwa miaka. Hii haimaanishi hawana uwezo. Ina maana tu kwamba wasaka ajira ni wengi kuliko nafasi zilizopo. Ndiyo maana ni muhimu kujifunza kuishi nje ya ajira rasmi bila kupoteza mwelekeo.

Baadhi ya wataalamu wanashauri, usikae nyumbani ukingoja kazi ifuate. Jitafutie shughuli za kukuza uwezo: soma, fanya utafiti, jiendeleze mtandaoni, au tengeneza mradi mdogo. Kujishughulisha hukuzuia kukata tamaa na hukujenga taratibu.

Katika kipindi hiki kigumu, mtandao wa watu (network) ni hazina isiyo na kifani. Wengine wanapata nafasi kwa kupigiwa simu tu. Hii sio bahati, bali ni matokeo ya kujenga uhusiano mzuri na watu muhimu. Tengeneza mtandao kupitia LinkedIn, kupitia marafiki, waliokutangulia, wahadhiri, au hata kupitia shughuli za kujitolea. Usiwe mtu wa kukaa kimya; onyesha kuwa upo tayari kushirikiana, kujifunza na kuchangia.

Kati ya siri zinazowasaidia wahitimu wengi ni kufanya kazi za kujitolea. Hapa unajenga uzoefu, unapata watu wa kukutaja, na unathibitisha uwezo wako. Watu huajiri wale wanaowaona wakifanya kazi, si wale wanaosubiri tu. Kujitolea pia kunaonyesha kwamba unaweka thamani mbele ya malipo—na mara nyingi, malipo huzifuata thamani.

Pia ni muhimu kujiuliza: kuna ujuzi gani wa ziada ninaoweza kujifunza? Ujuzi wa kompyuta, uandishi, uwasilishaji, matumizi ya takwimu, au hata lugha mpya vinaweza kukupa nafasi zaidi ya wengine. Kadri unavyopanua ujuzi, ndivyo unavyoongeza thamani yako sokoni.

Mwisho, jifunze bila kukoma. Uhitimu wa chuo ni mwanzo tu wa safari ya kujifunza. Dunia ya ajira inabadilika haraka, na wale wanaojifunza kila siku huwa mbele ya wengine. Soma vitabu, fuatilia kozi mtandaoni, uliza maswali, na endelea kujijenga.

Kwa kifupi, safari ya kutafuta ajira si rahisi. Lakini kwa malengo sahihi, utafiti makini, wasifu wenye nguvu, mazoezi ya mahojiano, kujitolea, kujenga mtandao, na kujifunza kila siku, utaweza si tu kuingia kwenye soko la ajira—bali pia kujijengea msingi imara wa maisha ya kitaaluma. Kila hatua unayopiga ni uwekezaji katika kesho yako.